

MPANGO WA UMILIKI WA HISA KWA WAAJIRIWA 2026

I'M IN!

KUTOKA TAREHE 10 JUNI
HADI 24 JUNI



L'ORÉAL


Matamano ya L'Oréal ni kufanya umiliki wa hisa kwa wafanyakazi upatikane kwa upana zaidi kutoka 2026. Kwa kukupa fursa ya kuwekeza katika hisa za L'Oréal kila mwaka¹, unaweza kuwekeza kwa kasi yako mwenyewe.

FAHAMU KUHUSU MPANGO WA L'ORÉAL'S WA UMILIKI WA HISA KWA WAAJIRIWA

Mpango wa L'Oréal wa Ununuzi wa Hisa kwa Wajiriwa hukupa fursa ya kushiriki katika faida za ukuaji wa Kampuni kwa kuwa mmiliki wa hisa kwa masharti ya upendeleo.

JE, NANI ANAWEZA KUSHIRIKI?

Wafanyakazi wote walioajiriwa kwa miezi 12 mfululizo katika Kampuni ya L'Oréal kufikia tarehe 24 Juni 2026 na ambao bado watakuwa wameajiriwa tarehe 24 Juni 2026.



JE, FAIDA ZA MPANGO HUU WA 2026 NI GANI?

1 PUNGUZO LA ASILIMIA 20 KWENYE BEI YA REJELEO YA HISA.

Bei ya usajili itawekwa tarehe 5 Juni 2026 na itakuwa sawa na bei ya marejeleo kisha kuondoa punguzo la asilimia 20. Bei ya marejeleo ni wastani wa bei ya ufunguzi wa hisa ya L'Oréal kwenye soko la hisa iliyowekwa kati ya tarehe 8 Mei na 4 Juni 2026 (imejumuishwa).

2 HADI HISA 3 ZINAZOTOLEWA NA L'ORÉAL



Kwa usajili wa	+	L'Oréal itachangia katika 2031	=	Jumla ya kiasi cha uwekezaji wa mwaka wa 2031
Hisa 1		Hisa 1		Hisa 2
Hisa 2		Hisa 1		Hisa 3
Hisa 3		Hisa 2		Hisa 3
Hisa 4		Hisa 2		Hisa 6
Hisa 5		Hisa 2		Hisa 7
Hisa 6 na zaidi		Hisa 3		Hisa 9 na zaidi

Utapokea hisa zinazotolewa chini ya mchango wa kulinganisha mwishoni mwa kipindi cha kufungwa, karibu na tarehe 31 Julai 2031, mradi wewe ni mwajiriwa wa Kampuni ya L'Oréal katika tarehe hiyo.

Kwa hisa 6 au zaidi zitakazonunuliwa, utapokea kiwango cha juu zaidi cha mchango wa kulinganisha wa hisa 3.

3 MIGAO UNAYOWEZA KUPATA

Utafaida kutokana na migao unayoweza kulipwa kila mwaka. Migao hii itawekezwa upya kiotomatiki katika *Fonds Commun de Placement d'Entreprise* ("FCPE" au Employee Shareholding Fund) na itaongezwa kwa asilimia 10 pindi tu unapokuwa na hisa zao kwa miaka miwili kamili ya kalenda.



¹ Ofa za umiliki wa hisa za siku zijazo zitategemea idhini ya mapema ya wanahisa wa kampuni na Bodi ya Wakurugenzi, idhini ya mamlaka husika, haswa AMF nchini Ufaransa, ukamilishaji wa taratibu zinazohitajika na wawakilishi wa wafanyakazi na masharti ya soko na uchumi. Vilevile, masharti yanayotolewa yanaweza kutofautiana mwaka hadi mwaka.

TAFADHALI KUMBUKA HILI KABLA HUJAWEKEZA

KWA KUSHIRIKI KATIKA MPANGO HUU, UTAKUWA MWANAHISA WA L'ORÉAL²

Uwekezaji wako unalingana na bei ya hisa ya L'Oréal na unategemea mabadiliko ya bei ya hisa ya L'Oréal. Kwa hiyo huwa hatari ya kupoteza mtaji.

UWEKEZAJI WAKO UTAFUNGWA HADI MIAKA 5

Uwekezaji wako utafungwa hadi tarehe 31 Julai 2031, isipokuwa katika hali za kuondoka kwenye kampuni mapema (Hali hizi zimetajwa katika hati ya "Nyongeza ya Nchi Yako").

Utapokea hisa zinazotolewa chini ya mchango wa kulinganisha mwishoni mwa kipindi cha kufunga, karibu tarehe 31 Julai 2031, mradi tu wewe ni mwajiriwa wa L'Oréal Group tarehe hiyo (isipokuwa vinginevyo ibainishwe katika Sheria za *Plan d'Attribution Gratuite d'Actions* (PAGA au Sheria za kushiriki bila malipo)).

TAFADHALI KUMBUKA KUWA KWA NCHI ZILIZO NJE YA UKANDA WA EURO:

■ Kwa vile hisa ya L'Oréal inaorodheshwa katika Euro kwenye Soko la Hisa la Paris, kipindi chote cha uwekezaji wako thamani ya uwekezaji wako itatofautiana kulingana na mabadiliko ya kiwango cha ubadilishaji kati ya Euro na sarafu yako. Hii inamaanisha kuwa Euro ikiongeza thamani dhidi ya sarafu yako, thamani ya hisa katika sarafu yako itapanda. Kinyume chake, Euro ikipoteza thamani dhidi ya sarafu yako, thamani ya hisa katika sarafu yako itashuka.

Ada za kudumisha akaunti zitalipwa na L'Oréal.



JE, UNGEPENDA KUSHIRIKI?

1

INGA KATIKA
INVEST.LOREAL.COM

2

BOFYA KITUFE
CHA «KUJISAJILI

3

INGA KWA MAELEZO
YAKO YA KUINGIA

4

FANYA MACHAGUO YAKO KWA
KUKAMILISHA SKRINI YA USAJILI

5

USISAHAU KUTHIBITISHA
USAJILI WAKO

Usajili mmoja pekee kwa kila mwajiriwa unaidhinishwa

² Si moja kwa moja kupitia FCPE ya "Mpango wa Umiliki wa Hisa kwa Wajiriwa wa L'Oréal".
³ Kiasi hiki kinaweza kupunguzwa ikiwa mpango utapokea usajili mkubwa.



USAJILI WA CHINI ZAIDI

HISA 1 YA L'ORÉAL



USAJILI WA JUU ZAIDI

HISA 20 ZA L'ORÉAL³ HADI ASILIMIA 25 YA MSHAHARA
WAKO WA MWAKA WA 2026 KABLA
YA MAKATO.

INGIA KWENYE

ili kupata maelezo zaidi kuhusu ofa
kwa mifano ya uwekezaji
ili kujisajili kuanzia tarehe 10 hadi
24 Juni 2026



invest.loreal.com



L'ORÉAL